- ***Mwadhama Protase Kardinali Rugambwa, Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu Katoliki la Tabora;***
- ***Mwadhama Polycarp Kardinali Pengo, Askofu Mkuu Mstaafu wa Jimbo Kuu Katoliki la Dar es salaam;***
- ***Mhashamu Gervas Nyaisonga, Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu Katoliki la Mbeya na Rais wa Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC);***
- ***Mhashamu Beatus Kinyaiya, Askofu Mkuu - Jimbo Kuu Katoliki la Dodoma;***
- ***Mhashamu Askofu Mkuu Angelo Accattino, Apostolic Nuncio to Tanzania;***
- ***Wahashamu Maaskofu Wakuu; Maaskofu wote ikijumuisha wastaafu;***
- ***Mhashamu Askofu Wilbroad Henry Kibozi, Askofu Msaidizi wa Jimbo Kuu Katoliki la Dodoma aliyepewa na Papa Makao ya Zallata;***
- ***Wahe. sana Mapadre, Mashemasi na Watawa mliopo;***
- ***Wahe. Mawaziri na Wabunge,***
- ***Mhe. Rosemary Senyamule - RC Dodoma, pamoja na viongozi wote wa Serikali, CCM na Vyama vingine vya Siasa;***
- ***Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama;***
- ***Wageni waalikwa na Watu wote wenye mapenzi mema.***

**Tumsifu Yesu Kristu... Mungu ni Mwema...**

Leo ni siku ya pekee sana kwa Kanisa Katoliki na hususan Jimbo Kuu Katoliki la Dodoma, ambapo tumejaliwa kushiriki ibada ya Misa Takatifu ya kumweka wakfu Askofu Wilbroad Henry Kibozi, Askofu Msaidizi wa Jimbo Kuu Katoliki la Dodoma. Kwa sababu hiyo, nami pia nawaomba tuungane kwa pamoja kumshukuru Mwenyezi Mungu na tumpigie makofi ya shangwe, vigelegele, nderemo na vifijo.

***Wahashamu Maaskofu, Mapadre, Watawa, Waamini na Wageni Waalikwa;***
Ninawaletea salamu za Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye ndiye aliyealikwa kuwa Mgeni Rasmi katika Ibada hii maalum. Rais Samia alipenda sana kushiriki katika ibada hii, lakini kutokana na majukumu mengi aliyonayo, amenituma kumwakilisha. Mhe. Rais na Serikali nzima tunakupongeza sana Mhashamu Baba Wilbroad Kibozi kwa kuwekwa Wakfu kuwa Askofu siku hii aliyoifanya Bwana, na tunaungana na jamii nzima ya Waamini na Watanzania wote kukutakia afya njema na utume mwema.

***Wahashamu Maaskofu, Mapadre, Watawa, Waamini na Wageni Waalikwa;***
Nilipopata maelekezo ya kuja kumwakilisha Mheshimiwa Rais, nilimuuliza kama ana ujumbe mahsusi zaidi ya pongezi. Nikajibiwa kwamba: "kaseme kadri Mungu atakavyokuongoza". Basi, katika kufanya maandalizi, nilianza kwa kupekua wasifu wa Mhashamu Askofu Kibozi nikakuta wasifu ulioshiba! Kumbe, hakuwa tu Padre mtaratibu, niliyekutana naye kwa mara ya kwanza eneo la Zanka hapa Dodoma akiwa amepata ajali ya gari, bali ni msomi bobezi, mwenye shahada ya uzamivu (Ph.D) katika *Dogmatic Theology* na tena wakati anateuliwa na Baba Mtakatifu alikuwa Profesa na Makamu wa Gombera, Seminari Kuu ya Familia Takatifu, Kahama. Kuona hivyo, jasho likanitoka nisijue nitasema nini la kufaa mbele yake

na mbele ya viongozi wangu wa Kanisa, Wasomi wa hali ya juu wasiojikweza. Hata hivyo, kwa kuwa sina budi kutoa salamu, naomba kusema yafuatayo:

**Kwanza,** kazi ya uchungaji kwenye Jimbo kubwa kama hili la Dodoma si nyepesi. Nina hakika ni ngumu na imejaa vikwazo vingi. Anayedhani vinginevyo, amuulize Baba Askofu Mkuu Beatus! Lakini, naomba nikuambie Mhashamu Askofu Kibozi, usiogope. Mwenyezi Mungu mwenyewe ndiye atakaye kuongoza na kukuwezesha. Kama ilivyoahidiwa katika kitabu cha Nabii **Isaya (42:6)** *..."Mimi Bwana, nimekuita katika haki, nami nitakushika mkono, na kukulinda, na kukutoa uwe agano la watu, na nuru ya Mataifa."* Tena tunasoma katika Waraka kwa **Waebrania (5:4)** : ..."*Na hapana mtu ajitwaliaye mwenyewe heshima hii, ila yeye aitwaye na Mungu, kama vile Haruni"*.

***Wahashamu Maaskofu, Mapadre, Watawa, Waamini na Wageni Waalikwa;***

Jambo la **pili**, nilipekuapekua vitabu mbalimbali ili kujua kidogo juu ya Mtakatifu Somo na mwombezi wa Askofu Kibozi. Nikashangaa kujua kwamba kumbe naye alikuwa Askofu! Sasa ninyi wazazi wenzangu, yafaa tujifunze kuwapatia watoto wetu majina yenye baraka na kuwasaidia kwenye wito wao. Mfano, ukimuita mtoto jina Protase, huyo atakuwa Kardinali kwa neema ya Mungu! Akiwa Beatus, atakuwa Askofu Mkuu; na akiitwa Filipo, naamini atakuwa mtumishi mwaminifu wa Serikali! Tunawashukuru sana wazazi wa Askofu Wilbroad kwa kumchagulia jina jema na kumlea vizuri. Lakini pia nilibaini kuwa, Mtakatifu Wilbroad Askofu, alisoma kwa bidii, na akapiga hatua kubwa katika maarifa ya dini na jamii, alifanya utume wa kimisionari akihubiri Injili katika nchi za Uholanzi na Denmark. Aidha, alijenga makanisa na kuanzisha Monasteri. Upendo na uvumilivu wake uliwavuta wengi kwenye dini ya Kikristo. Kwa kifupi, mimi naona ni ajabu kweli, kuwa Askofu wetu mpya anatembea akifuata nyayo za Somo wake! ikiwemo nidhamu mahali popote alipopita, mwalimu wa habari njema, na mtekelezaji hodari wa wajibu wake kama Padre. Ninawasihi walei wenzangu na wakleri tumuombee Askofu wetu mpya karama zaidi za imani, matumaini, mapendo kwa Mungu na jirani zake, hekima, haki, kiasi na ujasiri hasa wa kufundisha siri za Kristo.

***Wahashamu Maaskofu, Mapadre, Watawa, Waamini na Wageni Waalikwa;***

Jambo la **tatu**, napenda kuwasilisha shukrani za dhati za Serikali kwa Kanisa, kwa huduma bora mnazotoa kwa jamii ya Watanzania bila ubaguzi, hasa katika sekta za afya, elimu na malezi kwa vijana. Nafurahi kwamba baadhi ya huduma hizo zinatolewa kwa kushirikiana na Serikali. Mifano ni mingi, na kwa hapa Dodoma inajumuisha Hospitali ya Mt. Gemma, Shule ya Sekondari ya Wasichana Huruma, Kituo cha Kulea Watoto Yatima na Watu Wenye Mahitaji Maalum, Hombolo na pia Seminari, kama Bihawana ambazo zimelea watu wengi wakiwemo baadhi ya Watumishi wa Serikali ambao waliishia njiani kwenye wito wa upadre, kama mimi! Ninawahakikishia kwamba Serikali inathamini sana mchango mkubwa wa Kanisa Katoliki, na madhehebu mengine ya Dini, katika utoaji wa huduma hizo za kijamii na malezi bora. Aidha, Serikali inawahakikishia kuwa itaendelea kusimamia na kulinda haki ya kuabudu kwa wananchi wote kwa mujibu wa Katiba ya JMT, na kwamba wananchi wanaendelea kuishi katika mazingira ya haki na amani. Naliomba Kanisa Katoliki na madhehebu mengine ya Dini, kuendelea kuiunga mkono Serikali ili kwa pamoja tuweze kutoa huduma kwa Watanzania kama iwapasavyo watoto wa Mungu. Nasi kwa upande wa Serikali tutaendelea kuunga mkono jitihada za madhehebu ya Dini zote kutoa huduma kwa

jamii. Kwa mfano, hivi sasa tunashughulikia ombi la msamaha wa kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwenye mradi wa ujenzi wa Jengo la Afya ya Mama na Mtoto, Hospitali ya Mt. Gemma ambapo taratibu za msamaha huo zinafanyiwa kazi, japo zimechelewa, ili kukidhi matakwa ya kisheria.

***Wahashamu Maaskofu, Mapadre, Watawa, Waamini na Wageni Waalikwa;***
Napenda kuhitimisha salamu za Serikali kwa kusisitiza mambo manne.

**Mosi,** ni kuhusu changamoto za malezi na makuzi ya watoto zinazosababishwa na mambo mengi, ikiwemo matumizi mabaya ya maendeleo ya teknolojia ya habari na mawasiliano, na mwingiliano holela wa mila na desturi za mataifa mbalimbali. Mathalan, moja ya matokeo hasi ya matumizi mabaya ya TEHAMA ni kudhoofika muunganiko (*bond*) wa kindugu au kirafiki kati ya wazazi/walezi na watoto wao, ambao umepelekea watoto kukosa upendo na ulinzi wa wazazi/walezi. Vilevile, ukatili unaowezeshwa na mitandao unatishia usalama wa watoto, ambapo watoto wanarubuniwa ili kujihusisha na vitendo viovu. Naomba sana wazazi/walezi kutenga muda kujenga urafiki na watoto, ili kufahamu maendeleo yao, marafiki zao, na kuwawezesha kuwa huru kueleza changamoto zozote wanazopitia na hivyo kuweza kuwasaidia mapema. Malezi bora kwa watoto wetu ni muhimu sana ili kujenga Taifa bora na lenye ustawi. Kama ilivyoandikwa katika Kitabu cha **Mithali (22:6)**:*..."Mlee mtoto katika njia impasayo, naye hataiacha, hata atakapokuwa mzee"*. Tena, malezi yaguse nyanja zote za maisha ya mtoto, kimwili, kijamii, kitamaduni, kimaadili na kidini.

**Pili,** Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, alitufundisha kuwa "*kazi ni kipimo cha utu*". Mwalimu alisisitiza sana Watanzania kufanya kazi ili kujipatia kipato kwa njia halali. Lakini, hivi sasa wapo vijana wengi wenye umri wa kufanya kazi wasiojishughulisha na kazi yoyote ili kujikimu kimaisha, kiasi kwamba wamekuwa tegemezi! Ukiacha watoto, wazee na wenye ulemavu, mtu yeyote akiwa tegemezi, hadhi ya utu wake inapungua mbele ya jamii. Hivyo, napenda kutumia hadhara hii kuwahimiza vijana kufanya kazi kwa bidii ili kujipatia kipato kitakacho wawezesha kujikimu kimaisha. Vilevile, nawasihi vijana kutochagua mno kazi. Hivi sasa, kazi nyingi za staha ziko kwenye kilimo cha mbogamboga na matunda, na ufugaji wa wanyama, aina mbalimbali za ndege, na viumbe maji. Hii inahitaji nidhamu ya kazi na kujituma. Biblia Takatifu katika kitabu cha 2 Wathesalonike ***(2 Wathesalonike 3:12),*** inatuhimiza kufanya kazi *"...Basi twawaagiza hao, na kuwaonya katika Bwana Yesu Kristo, watende kazi kwa utulivu na kula chakula chao wenyewe"*.

**Tatu*,*** sambamba na msisitizo wa kufanya kazi halali, naomba kuwasisitiza Watanzania wote kuhusu matumizi ya rasilimali muda. Kwa bahati mbaya Watanzania wengi hatuthamini muda na tunautumia vibaya! Lakini, ukweli ni kuwa muda ni rasilimali muhimu sana ambayo ukiipoteza au kuichezea haiwezi kurejeshwa. Aidha tumekuwa hatuzingatii muda katika miadi au matukio mbalimbali na hata katika utoaji huduma kwa jamii. Tunapoteza muda mwingi wa kuzalisha mali au kutoa huduma na hivyo kupunguza kasi ya ukuaji wa Pato la Taifa na la mtu mmoja mmoja. Mt. Josemaria Escriva, Mwanzilishi wa Jimbo la Msalaba Mtakatifu la Kazi ya Mungu *(Opus Dei)* alituasa katika kitabu chake *(Njia: 13 – 14)* kwamba: *" Tupilia mbali mawazo yanayokufanya upoteze muda wako. Usipoteze nguvu zako na muda wako ambao ni mali ya Mungu..."* Aidha, katika Kitabu cha **Marko (1:35)** tunaona jinsi Yesu alivyotumia vizuri muda wake, nanukuu *"...Hata alfajiri na mapema sana akaondoka, akatoka akaenda zake mahali pasipokuwa na watu, akaomba huko."* Baada ya hapo

aliendelea na kazi yake ya kuhubiri katika Masinagogi na katika nchi yote ya Galilaya. Hilo litufundishe kwamba kuna tija zaidi kufanya mazoea ya kuamka alfajiri kuanza na sala kabla ya kuanza kazi. Ninawasihi Waamini wenzangu na Watanzania kwa ujumla kuthamini, kutunza na kutumia muda vizuri katika kila jambo tunalofanya. Ndiyo sababu zamani Mkristo Mkatoliki akienda misa kwa kuchelewa, akakuta liturjia ya Neno imepita, tuliagizwa tusipokee ekaristi takatifu na tusubiri misa inayofuata. Naona siku hizi hata hili hatulizingatii ipasavyo!

**Nne,** napenda kutumia nafasi hii kuwakumbusha Watanzania wote wajibu wetu wa kufanya usafi, pamoja na kuheshimu, kupenda na kutunza mazingira. Ni dhahiri kuwa kutokana na shughuli zetu za kibinadamu, tumeharibu miti na uoto wa asili. Ninawasihi viongozi wa Dini, kwa mamlaka mliyopewa na Mungu, mtusaidie kuendelea kuhamasisha usafi, upandaji miti na utunzaji wa mazingira bila kuchoka. Nawaomba kwa unyeyekevu mkemee utupaji hovyo wa taka, uchomaji wa misitu na ukataji hovyo wa miti hususan kwa kutumi misumeno ya mnyororo *(chain saw)* ambayo imegeuka kuwa silaha mbaya ya kuangamiza misitu. Aidha, ninazikumbusha Taasisi zote za umma na za kidini (zikiwemo nyumba za Watawa, Seminari, Shule na Vyuo) ambazo zinalisha zaidi ya watu 100 kwa siku, kuhama kutoka matumizi ya nishati chafu, yaani mkaa na kuni, kwa ajili ya kupikia na kuanza kutumia nishati safi, yaani gesi asili, *bio gas* na umeme ili kufikia lengo la Taifa la 80% ya Watanzania wawe wanatumia nishati safi ya kupikia ifikapo 2034. Nawaomba Watanzania kutambua kwamba tumeidhuru sana nchi yetu na tayari sasa inatudhuru wenyewe kupitia uhaba wa maji, ukame, joto, mafuriko, maporomoko ya udongo, kutoweka kwa baadhi ya viumbe, kuongezeka kwa magonjwa na umaskini. Hivyo, nawasisitiza tujirudi na kuanza upya, tusingoje kuteketea kabisa.

***Wahashamu Maaskofu, Mapadre, Watawa, Waamini na Wageni Waalikwa;***

Kwa unyenyekevu naomba kumalizia kwa kuwakumbusha kuwa Kanisa na madhehebu mengine (ya kweli) ya Dini ndiyo dhamiri (*Conscience*) ya jamii. Hivyo, tunawatarajia viongozi wetu wa Dini kuishi wito wenu wa kinabii, mkisema na kuutetea ukweli kwa ajili ya maslahi ya wananchi, hasa wanyonge. Tena mfanye hivyo kwa uhuru, bila woga lakini bila kuathiri amani na umoja wa kitaifa. Aidha, nawasihi muendelee kuwakumbusha waamini na Watanzania kwa ujumla kwamba haki inaambatana na wajibu. Nawaomba pia msiache kuliombea Taifa letu ili liendelee kuwa na amani na utangamano, ikiwa ni pamoja na kutuombea sisi viongozi wa Serikali ili tutekeleze majukumu yetu ya kuwatumikia Watanzania kwa unyenyekevu na bila upendeleo. Naomba pia nitoe pongezi kwa Baba Paroko wa Parokia ya Miyuji-Mbwanga, Halmashauri ya Walei Jimbo na Parokia na wote wanaohusika kwa maandalizi mazuri ya sherehe hii, kwaya na nyimbo nzuri, mahubiri mazuri, na mahudhurio mazuri ya waamini na wageni waalikwa. Aidha natoa pongezi kwa hatua nzuri iliyofikiwa katika ujenzi wa Kituo cha Hija. Kabla sijaondoka hapa, naomba nitoe zawadi ndogo kwa Askofu wetu mpya. Ninaomba pia kutamka ahadi ya Mhe. Rais ya kuchangia ujenzi wa Kituo hiki cha hija (Tsh. 50,000,000) na kiasi kama hicho tena kwa ajili ya ujenzi wa Basilica unaoendelea pale Kizota. Kwa mara nyingine tena, tunakupongeza kwa dhati Baba Askofu Wilbroad Henry Kibozi kwa kuwekwa Wakfu na kukabidhiwa kazi ya Askofu Msaidizi wa Jimbo Kuu la Dodoma. Serikali inakuahidi ushirikiano wa dhati kabisa katika utekelezaji wa majukumu yako. Tunakuombea baraka, afya njema na mafanikio katika utume wako.

***Tumsifu Yesu Kristu. Asanteni sana kwa kunisikiliza.***